# BILIONI 3.4 KUJENGA STENDI KIBAHA

***Na Innocent Byarugaba***

Halmashauri ya Mji Kibaha Mkoani Pwani inatarajia kuanza ujenzi wa Stendi Mpya ya Kisasa wiki hii itakayogharimu kiasi cha Tsh.3,478,561,971/= Mpaka kukamilika kwake.

Stendi hiyo inajengwa karibu na Kalakana ya Serikali eneo la UJENZI na inajengwa na Mkandarasi M/S GROUP SIX LTD ya Dar-es-Salaam kwa kipindi cha Miezi 6

Akizungumza na Mwandishi wa Habari hii, Msanifu Majengo wa Halmashauri ya Mji Kibaha Fortunatus Ndibalema amesema kuwa Stendi hiyo inajengwa kwenye eneo lenye ukubwa wa mita za Mraba 20,000 na itakua na uwezo wa Kuegesha Mabasi Makubwa 60, Mabasi Madogo 48, Bajaji 10 teksi pamoja na Bodaboda 20

Ndibalema ameongeza kuwa, kutakua na eneo maalumu kwa ajili ya Kuegesha zaidi ya Magari 80 ya watu wanaokuja kuwafuata ama kuwaleta abiria kituoni hapo kwa wakati mmoja.

"Pamoja na kuwa kituo hiki kitazungushiwa Ukuta, pia kitakua na Miundombinu ya vyoo, Kituo cha Polis, Kizimba cha kukusanyia taka na sehemu ya Kupumzikia Abiria. Aidha, kutajengwa Ofisi za Kukatia Tiketi, Mghahawa, Jengo la Utawala, Kituo cha Mafuta na Gereji" alisema na kuongeza

Akizungumza na Wataalam wa Halmashauri ya Mji Kibaha kwenye Kikao cha Kamati ya Fedha, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kibaha ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Msangani Mheshimiwa Leonard Mlowe amesema kuwa pamoja na kutoa huduma kwa Wananchi pia kitakuwa chanzo endelevu cha Mapato ya Halmashauri hivyo amesisitiza kujengwa kwa wakati na ubora ili kuwaondolea kero wananchi wanazozipata kwenye kituo cha sasa hasa kipindi hiki cha mvua

Hii stendi kubwa ni ya kwanza kujengwa tangu Halmashauri ya Mji Kibaha kuanzishwa rasmi mwaka 2008 na itakamilika Mwezi Oktoba Mwaka huu.